

## **DIBAJI**

Zamani tulikuwa tunasimuliwa hadithi za MTU kaenda msituni na kukutana na zimwi na zimwi likampa MTU huyo kidani na kumwambia kila atakachosema kwa kidani hicho atapata. MTU huyu akitamka "nataka nyumba ya ghorofa" inatokea na anaipata. Akisema "nataka gari" inatokea. Yaani hadithi hizi sijui zilikuwa na lengo gani. Hizi zilitengeneza picha katika akili za watoto kwamba kuna vitu vinaweza kupatikana pasipo juhudi.

Maisha yangekuwa na ujanja ujanja wa kufikiri tu na kutamka basi unachotaka kinatokea basi dunia ingekuwa sehemu ya vurugu tu. Picha inayokuja katika akili yako inatengenezwa na mawazo yako. Mawazo uliyo nayo yanajengwa na kile unachokiona, kile unachokisikia, kile unachokisoma. Hii "picha" au "taswira" ndiyo inaleta NDOTO.

Ndoto hii sasa, ndio mwandishi wa kitabu hiki, Joas, anaiandikia katika namna ya kutoa ahadi madhubuti anasema NITATIMIZA NDOTO YANGU. Kuna changamoto nyingi unazozoweza kupitia mpaka kufikia ndoto yako (mahali unapotaka kuwa au mtu unayetaka kuwa). Moja ya changamoto kubwa ni pale wewe mwenye ndoto unapomshirikisha MTU asiyekuwa na hiyo ndoto yako. Kwa bahati mbaya kabisa unakuta huyo MTU aliwahi kufanya jambo linalofanana na ndoto yako na kushindwa au anajua MTU aliyewahi kufanya jambo hilo akashindwa. MTU wa namna hii ana uwezo mkubwa wa kukukatisha tamaa na kukufanya uishie njiani kabla ya kufika katika kilele cha mafanikio yako. Joas, katika kitabu hiki, anakukumbusha ahadi yako ya kutimza ndoto hiyo na ukae ukijisemea moyoni na hadharani kuwa NITATIMIZA NDOTO YANGU.

Pamoja na hilo pia unajikuta ile picha uliyo nayo kichwani mwako haifikiwi kama unavyotarajia kwa kuwa una picha dhaifu, una ndoto ndogo. Katika kitabu changu kiitwacho Mafanikio Huanzia Kichwani Mwako, nimeandika juu ya ukweli kwamba ndoto yako haina budi kuwa kubwa na ya kukutisha

kabisa. Ndoto itakayotoa mwanga kwa wewe kujiandaa kwa nguvu na akili, ili kuitimiza. Ukiwa na matarajio madogo, unakuta akili yako inakosa shauku inayotosha kukusukuma mpaka kilele cha mafanikio hayo. Ukijenga picha kubwa basi kisaikolojia unajipa nafasi ya kuamini ukicheza tu na usipojituma vya kutosha basi ndoto yako haitatimia. Joas, anakupa mbinu zinazokupa shauku kubwa na isiyokoma katika kutimiza ndoto yako, hata kama ni ndoto kubwa kiasi gani.

Nikupongeze wewe uliyejali na kununua kitabu hiki. Hautajuta kukisoma. Kitabu hiki kikapate nafasi ya kubadilisha mawazo yako ambayo yataathiri matendo yako katika kuhakikisha unatimiza ndoto zako. Jambo hili ni kubwa na ambalo hufanywa na watu wachache na wanaojua kwamba shule haina mbadala. Kujifunza hakukomi kwa sababu ya kumaliza shule au chuo ila ni suala la maisha.

Nikutakie usomaji mwema na usisahau wakati wote kujituma na kufanya kazi kwa bidii na kujikumbusha kimoyomoyo na kwa sauti, ukijiambia "Nititimiza Ndoto yangu".

**Reuben Ndimbo - 0715436350**

**Mwenyekiti, Nafanikiwa Inspiration**